# Vita vya Sudan
# Hadithi ya Ukoloni, Usaliti na Udanganyifu

**"Hofu inayoendelea nchini Sudan haina mipaka"**
**Mkuu wa Shirika la UN la Haki za Binadamu, Volker**

**Mgogoro wa kikatili nchini Sudan kati ya Vikosi vya Wanajeshi wa Sudan vinavyoongozwa na Jenerali Abdel Fattah al-Burhan, mtawala mkuu wa Sudan, na Vikosi vya kijeshi vya Msaada wa Haraka vinavyoongozwa na Mohamed Hamdan Dagalo (Hemedti), naibu wa zamani wa Burhan katika Baraza la Utawala, sasa umeingia mwaka wa tatu. Baadhi ya makadirio yanaweka idadi ya waliouawa kuwa ١٥٠,٠٠٠, na ukatili wa kutisha uliofanywa na pande zote mbili, ikiwa ni pamoja na mauaji ya kinyama, mateso, na ubakaji mkubwa. Mauaji ya kikabila na kikatili pia yameripotiwa katika miji mbalimbali, vijiji na kambi za watu waliohama. Vita hivyo vimesababisha mzozo mkubwa zaidi wa kibinadamu, mzozo mkubwa zaidi wa wakimbizi, na janga kubwa zaidi la njaa ulimwenguni, huku nusu ya watu milioni ٥٠ wakikabiliwa na njaa.**

**"Janga hili la kibinadamu nchini Sudan "sio tu ni mgogoro, bali ni mgogoro wa sura nyingi unaoathiri kila sekta, kuanzia afya na lishe hadi maji, elimu na ulinzi."**

**Hata hivyo, mzozo huu umeelezewa kuwa "vita vilivyosahaulika" na "mgogoro uliofichwa na usioonekana" kwa sababu haujapata usikivu wa kimataifa na utangazaji wa vyombo vya habari vya kimataifa unaostahili. Mtume (saw) amesema: «مَثَلُ الْمُؤْمِنِينَ فِي تَوَادِّهِمْ وَتَرَاحُمِهِمْ وَتَعَاطُفِهِمْ مَثَلُ الْجَسَدِ إِذَا اشْتَكَى مِنْهُ عُضْوٌ تَدَاعَى لَهُ سَائِرُ الْجَسَدِ بِالسَّهَرِ وَالْحُمَّى» "Mfano wa waumini katika kupendana kwao, na kuonena huruma kwao, na kuoneana upole kwao ni kama mfano wa mwili. Pindi kiungo kimoja kinaposhitakia maumivu, mwili mzima huitikia kwa kukosa usingizi na homa ." Kwa hiyo, Kitengo cha Wanawake katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kimezindua kampeni ya kimataifa kuangazia maafa yanayozidi kuwa mabaya ya kibinadamu yanayowakabili Waislamu wa Sudan. Kampeni hii, yenye kichwa, "Vita vya Sudan: Hadithi ya Ukoloni, Usaliti na Udanganyifu" pia itashughulikia :**

- Siasa na Ajenda Fiche nyuma ya mzozo huu
- Dola za Kieneo na Kimataifa Zinazofadhili Vita hivi na Kwa Nini
- Historia ya Sudan na Mambo Yaliyosababisha Mizozo ya Hivi Karibuni na Kufeli Kiuchumi
- Kwa nini Mfumo wa Kidemokrasia Ufafeli Kutatua Maelfu ya Matatizo ya Kisiasa, Kiuchumi, Kiakhlaki na Kijamii Social
- Vipi Uongozi wa Kiislamu wa Dola ya Khilafah Unaweza Kujenga Mustakbali wenye Ufanisi, Usalama, na Mafanikio kwa Sudan na Ulimwengu wote wa Kiislamu

**﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ اسْتَجِيبُواْ لِلّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُم لِمَا يُحْيِيكُمْ﴾ [سورة الأنفال: 24]**




**﴿Enyi Mlio amini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapo kuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele﴾**

**#SudanCrisis**

HT-COM-WS | WSCMOHT1924 | WOMENSHARIAH5